

# **Jiografia Ya Biblia**

**Na Don Delukie**

**Mtafsiri Joshua Mwakyasima**

## **BIBLE GEOGRAPHY**

### **Utangulizi:**

- I. Kulikuwa na wakati ni kwa uchache sana au nchi chache sana zilikuwa zinafahamika, kuliko zile zote zilizofunuliwa na Biblia.
  
- II. Pamoja na matukio ya utaratibu wa kisasa wa:
  - A. Usafiri
  - B. Mawasiliano na
  - C. Vyombo vinavyobadiriha hasa halisi ya asili - vimechunguzwa sana
  - D. Wakati wote neno la Mungu limethibitisha
  
- III. Biblia wakati wote ni sahihi na haina makosa ikiwa nipamoja na:
  - A. Maarifa -Ebr. 4:12.
  - B. Wakati
  - C. Ramani
  - D. Jedwali
  - E. Picha za rangi.
  
- IV. Darasa hili litafurahia kwa ufahamu tutakaopata kwa kuzijua sehemu mbalimbali Kijiografia.
  
- V. Ni kwa nini tunajifunza Jiografia ya Biblia? Ni kwa sababu tunaongeza ukubwa wa ufahamu wetu juu ya Biblia.
  - A. Kama ukisikia mji fulani wa zamani, ambao hujawahi kufika na kama Hujui ni wapi upo utakuwa na hamu ndogo tu kutaka kuelewa juu yake.
    1. Inakuwa kinyume na kama umeyasikia mambo ya zamani yaliyowahi kuchukua nafasi pale - utakuwa na hamu sana.
  - B. Wengine wamelipuunzia sana somo hili la Jiografia ya Biblia matokeo yake Watu hawa wanajidanganya wenyewe na kushindwa kulifurahia neno la Mungu kama lilivyo, na kushindwa kuhubiri vuzuri neno la Mungu.
  - C. Utakapojifunza somo hili utaiona Biblia ikiwa ina kuja kwako ikiwa hai:
    1. Sio kozi ya vitu visivyo fahamika.
    2. Utaona zile sehemu unazosisikia kama sio kweli, kuwa ni kweli.
  - D. Tujiandae vizuri kwa ajili ya kujifunza kozi hii, utakuwa na utajiri mkubwa wa ufahamu, juu ya kitabu cha ajabu kuliko vyote duniani Biblia.

### **SOMO LA KWANZA.**

#### **Ulimwengu wa Agano la Kale.**

- I. Katika hali ya Kiroho Palestina au Kanaani ni Nchi ya Wakristo na Wayahudi vilevile.
  - A. Matukio ya KiBiblia kihistoria yalichukua nafasi huko katika ulimwengu wa Agano la Kale.
    1. Historia hiyo imeendelea kuwa changamoto kwa mwanadamu na ujumbe wa Mungu tuliopewa.
    2. Mwanadamu ni kiumbe kinachohitaji Nafasi na Muda. Kwa hiyo

Jiographia na Historia lazima viongezwe.

PALESTINA MAHALI ILIPO, (ISRAELI)

- II. Palestina (Kanaani) ipo pembezoni mwa Bahari ya Mediteranea pwani ya mashaariki
- A. Kuna njia au barabara nyingi za kibiashara kuingia na kutoka Afrika na Ulaya na Asia yote.
  - B. Wakati wote umuhimu wa Palestina umejitokea.
    1. Katika Agano la Kale.
    2. Katika Agano Jipya.
  - C. Imekuwa na majirani ambao ni waarabu na kumekuwa na ugomvi wa muda mrefu kati ya Taifa hili na Waarabu hivyo imekuwa n isababu ya hofu ya Kule mashariki ya kati nzima.
  - D. Mataifa ya sasa ya mashariki ya kati yanajitahidi kujenga Nchi hiyo tasa kuwa atakufikia Nchi ijaayo "Maziwa na asali".
- III. Bahari Zinazopatikana Ulimwengu wa Agano la Kale.
- A. Mediteranea: (Bahari kuu).
    1. Kuna njia muhimu mno za baharini .
    2. Ni mpaka wa Palestina kwa upande wa Magharibi, Yos.1:4.
    3. Kuna bandari ya Joppa au Jaffa kwa sasa Tel Aviv.
  - B. Ghuba la Uajemi.
    1. Ipo mashariki mwa Peninsula ya Uarabuni.
    2. Waandishi wengi wanasema Bahari hii ya Ghuba ya Persia imesababishwa na mito miwili Tigris na Frati.
    3. Mji wa Uru. Ulikuwa maili 100 kutoka katika kichwa cha hii bahari hapo zamani.
  - C. Bahari ya Kaspiani.
    1. Bahari kubwa kabisa ulimwenguni iliyozungukwa na Nchi kavu.
    2. Maji yake ni ya chumvi.
- IV. Bahari ya Shamu Au Bahari Nyekundu.
- A. Maji mengi yaliyo katika ufa wa bonde Yordani.
  - B. Ni mpaka kati ya Africa na Uarabuni.
  - C. Imezungukwa pande zote na Jangwa
- V. Bahari Nyeusi.
- A. Ni mpaka kati ya Ulaya na Asia.
  - B. Haionekani popote katika Agano la Kale.
- VI. Bahari Ufi (Chumvi)
- A. Bahari hii ni bahari ambayo maji yake yako chini sana.
  - B. Pia imeitwa
    1. Bahari ya Chumvi, Mwa. 14:3.
    2. Bahari ya Araba, Kum. 3:17.
    3. Bahari ya Mashariki, Yoeli 2:20.

Mito Muhimu ni Mitano.

I. Tigris

- A. Jina lingine unaitwa Hidekeli, Mwa.2:14.
- B. Unatokea kwenye miinuko ya Armenia katika Asia ndogo na kuishia katika Bahari ya Ghuba la Persia.
- C. Wakati wa zamani umuhimu wa miji ya Assyria ya Ashuru na Ninawi ilikuwa ukingoni mwa mto huu.

II. Frati

- A. Chanzo chake ni mlima Taurus

III. Orente

- A. Unaanzia Lebanon milimani unaishia Bahari ya Mediteranea.

IV. Mto Nili

- A. Unaanzia Afrika mashariki katika ziwa Victoria au Nyanza mpaka Bahari ya Mediteranea Misri.
- B. Mto ulioleta ustaarabu wa Misri.
- C. Wamisri waliufikiria mto huu kuwa Mungu.

V. Yordani

- A. Ni mto mkubwa zaidi kule Palestina (Israeli)
- B. Unaanzia katika mlima Hermon na kuishia Bahari mfu kwa kupitia Ziwa Galilaya hapo ndipo inapotelea kwa jumla.
- C. Wakati mwingine ulijulikana kama mto wa Jangwani, Amo. 6:14; Yos. 12:2, Yoh. 3:23.

VI. Majina matano ya Nchi ya Israeli.

- A. Palestina
- B. Kanaani
- C. Ahadi
- D. Maziwa na Asali
- E. Takatifu.

Milima Mikubwa.

I.. Ararati- 14,000 fts kileleni 17, 000 fts.

- A. Mahali ambapo safina ya Nuhu ilipotua baada ya Gharika, Mwa. 8:4.
- B. Upo mashariki mwa Nchi ya Armenia kati ya Kaspiani na Bahari Nyeusi.
- C. Jina lingine kufuatana historia kuitwa Mlima wa Nuhu.

II. Zagros: 9000 FTS.

- A. Ni safu za milima mashariki mwa mto Tigris unatokea kaskazini kuenda kusini

- B. Zamani ulikuwa ni mpaka wa Ashuru na Umedi.
- III. Taurus: 12,250 fts.
  - A. Jina lingine ni Fedha - madini inayopatikana.
  - B. Kaskazini mwa mji wa Tarso.
- IV. Lebanoni (Milima) - 10,200 ft. urefu.
  - A. Milima hii inafanywa na maendelezo ya Taurus.
- V. Mlima Hermon - Kilele.
  - A. Maendelezo ya safu za milima ya Anti-Lebanoni uliyo upande wa pili wa miti Lebanoni.
- VI. Mlima Sinai.
  - A. Upo kusini katika Peninsula ya Sinai kati ya mfereji wa Suez na Ghuba la Agaba.
  - B. Hapa mdipo Musa alipopokea sheria kwa ajili ya wana wa Israeli. (Kut.20 ff)

## **SOMO LA PILI**

### **Utangulizi:**

- I. Tumekwisha elezea mambo huhimu katika ulimwengu wa Agano la Kale.
  - A. Miili mikubwa ya maji - Bahari.
  - B. Mito.
  - C. Milima.
- II. Sasa na tuendeleo kuangalia Nchi Jinsi zilivyokuwa zinaonekana.
  - A. Hizi ni sehemu zinazoleta kumbukumbu tunapozisikia.
  - B. Ni sehemu zilizoleta utaratibu kama tujuavyo.
    - 1. Zilikuwa na watu maarufu.
    - 2. Vilevile matukio makubwa yaliyotendeka huko.
    - 3. Baadhi yake Mungu alizitumia kukamilisha kusudi lake la milele, Efe. 3:10 -11.
- III. Tupo hapa sasa ni kwa sababu ya matukio yaliyochukua nafasi katika nchi hizo katika maelezo ya miaka mingi iliyopita.
- IV. Utakapoendelea kukua na kuzifahamu nchi hizo basi utaongeza ufahamu mkubwa katika kujifunza Biblia

### **Mwilli:**

- I. Historia fupi juu ya Mataifa.
  - A. Historia inagawanyika asili yake kama ilivyo Sayansi.
    - 1. Wengine walishikiria ustaraabu wa Mesopotamia sasa Irag.

2. Wengine walifiria ni Misri ya zamani.
3. Bado wengine kudai kuwa ustaarabu huu ni kutokea mashariki ya mbali kama ndiko asili ya mwanadamu.

## II. Mpangilio wa Mataifa.

### A. Yaliyotokana na wana watatu wa Nuhu, Mwa. 10.

1. Yapheti - Mataifa 7
2. Hamu - Mataifa 4, Mwa. 10:1.
3. Shemu - Mataifa 5

### B. Yaphet: (mst. 2-5).

1. Gomeri - Indo-Ulaya.
2. Magogu - Scyilians (Kas./Mash. Bahari Kaspiani)
3. Madai - Umedi (Kusini ya Kaspian)
4. Yavani - Ugriki (Mwisho wa kusini Balkan Peninsula)
5. Tubali - Haifahamiki.
6. Mesheki - Haifahamiki.
7. Tirasi - Thracians (Kati ya Uyanani na Bahari Nyeusi pwani)

### C. Hamu: Ungua (mst. 6-14)

1. Kushi - Ethiopia.
2. Misri - (Mizraim) - Misri
3. Putu - Libya.
4. Kanaani - Palestina (Israeli - Uyahudi)

### D. Shemu: Jina (mst. 21-31)

1. Elamu - Waelamu (Kasi ya Uajemi na Mash. ya Bahari)
2. Ashuru - Assyria (Kusi Magh - Asia)
3. Arfaksadi - Ukalidayo (Tigrisi na Ufrati chini)
4. Ludi - Lyalia (Magh - Asia ndogo)
5. Aramu - Shemu (kati ya Ashuru na Kanani)

## III. Nchi kubwa za Kibilia ni Tatu.\_

- A. Armenia - Nchi ya zamani ambapo safina ilitua, 2 Fal. 19:37; Isa. 37:38.
- B. Mede - Mungu aliwatumia watu hawa kutimiza maandiko juu ya maandishi ukutani 2 Fal. 17:6; 18 :11; Dan. 5:25-31; 6:28.
- C. Ujemi - Ujemi na Umedi - ndizo zilizofuata kutawala dunia. Dan. 2:36-39; 7:5; 8:3; 11:2; Est. 1:3.
  1. Nchi zilizowahi kutawala dunia yote kila moja kwa wakati mmoja.
    - a. Misri.
    - b. Ashuru.
    - c. Alexander wa Makedonia, (Ulaya).
    - d. Babeli.
    - e. Umedi na Uajemi.
    - f. Rumi.
  2. Dira ya mwelekeo wa dunia:

## Kaskazini

Magharibi

Mashariki

## Kusini

## D. Duniani kuna Mabara 7.

1. Afrika.
2. Marekani ya Kaskazini.
3. Marekani ya Kusini.
4. Asia.
5. Australia
6. Antartica
7. Ulaya.

## E. Kuna bahari kubwa 4 Duniani.

1. Uhindi.
2. Arctic.
3. Pacific.
4. Atlantic.

## F. Historia ya Agano la Kale inachukua mabara mawili tu kati ya Saba.

1. Afrika - Kaskazini Afrika (Kas. na Kas. Mash.)
2. Asia - Asia Ndogo.

## G. Historia ya Agano Jipya iko katika mabara 3 kati ya saba.

1. Afrika - Afrika Kaskazini.
2. Asia - Asia Ndogo
3. Ulaya.

Nchi zilizokuwa wazi ni 5.

1. Sumer - Sehemu ya zamani ya Babeli, Mwa. 14:1; 11:31, Dan. 1:1
2. Ashuru - Kati ya Babeli, Armenia, na Umedi - Tigri Mto, Mwa. 2:14; 25:18  
Yoh. 1:2.
3. Mesopotamia - sehemu ya wazi kati Tigris na Ufrati, Mwa. 24:7 -10
4. Elamu - Kaskazini ya Ghuba ya Uajemi, Mwa. 10:23.
5. Arabu - Peninsula kati ya Afrika na Asia, 1 Fal. 10 :15; 2 Nya.17:11, Ez. 27:21.

Nchi zilizo zunguka mashariki mwa Bahari ya Mediterania 6.

1. Asia ndogo - ilijumuisha falme:
  - a. Lidia.

- b. Ashuru
- c. Hiti
- 2. Shemu mji mkuu ni Damaskus kwa Kiebrania - Aram.  
Ilikuwa katika Ashuru na kanaani, 2 Sam. 8:6; 15:8; Ez. 17:16; Lk. 2:2; Mdo. 15:23, 41.
- 3. Kanaani - Mabaki ya chini ya meditranea pwani na Bonde la Yordani.
  - a. Mabaki ya wasio wayahudi wote, Mwa. 10:18 -20; Hes. 13:29; Josh. 11:3.
- 4. Phoeniki - Mstali mwemba Kaskazini mwa mlima Karmel walizungumza Semitic lugha.
  - a. Miji yake mikubwa ni Tiro na Sidoni.
- 5. Philistina - Jina hili linatoka Palestina kuonyesha Nchi walipewa Waisrael Yoe.3:4; Ebr. 11: 9; Zak. 2:12.
- 6. Misri - Nyumba ya utumwa kwa Israel.
  - a. Nchi yenye rutuba kando ya mto Nili, Mw.12:10; 39:1; 42:1; 47:28; 29; Mdo. 7:23, 24.

#### Nchi ya Palestina au Kanani.

- I. Kanaani ni Jina lililotumika katika A.K. kwa nchi hiyo iliyokuwa katikati ya Yordani na Mediterania kusini ilipakana na jagwa.
- II. Kwa usahihi zaidi tunapozungumzia Palestina twaweza kuwa tunazungumzia mataifa mawili.
  - A. Nchi ya Wafilisti.
  - B. Nchi ziliyokaliwa na makabila 12 ya Israeli.
- III. Migawanyo Yake ya Asili.
  - A. Uwanda wa Pwani.
  - B. Ukanda wa katikati.
  - C. Bonde la Yordani.
  - D. Ukanda wa mashariki.
  - E. Ukanda wa Jangwa (Mbele ya mashariki).
- IV. Maji Yalivyo Katika Nchi ya Palestina.
  - A. Mto Yordani
  - B. Ziwa Hula.
  - C. Bahari ya Galilaya
  - D. Bahari Iliyokufa.
  - E. Mito mingine mingi midogo midogo.
- V. Milima Ya Palestina.
  - A. Tabor - Debora na Baraka walitayarisha .... Wakanaani.
  - B. Gilboa - Sauli na Jonathani walikufa vitani na Wafilisti.
  - C. Karmeli - Nabii Eliya aliwashinda manabii na makuhani wa Baali.
  - D. Ebal na Gerzimu-



1. Baada ya wana Waisraeli kushinda Yoshua .... Amoc na Musa
2. Baraka zilitangazwa - kutoka mlima Gelizimu.
3. Laana zilingazwa kutoka mlima Ebal, Kum. 11:29.
4. Mwanamke Msamaria, Yosh. 8:33-35, Yoh. 4:1
- E. Mlima Sayuni - kwa kawaida Sayuni lilikuwa ni Jina la Yerusalemu mji mtakatifu.
  1. Mashariki mwa Yerusalemu Mlima Olivet au Olivus. (Mlima wa Mizeituni).
- F. Mlima Hermon.
- G. Mlima Gileadi - Gidioni alikusanya Jeshi (Waa. 7:3)
- H. Mlima Nebo
  1. Mahali Musa alipotazama nchi Ahadi.
  2. Uko katika nchi ya Wamoabu.
  3. Mahali alipofia Musa.

#### VI. Njia kuu 3.

- A. Njia ya Pwani.
- B. Njia za majini.
- C. Njia kuu za wafalme.

### MABABA WALIVYOSAFIRI.

#### Utangulizi:

- I. Maelezo ya mapema kabisa ya Biblia kuhusu Maisha ya Mwanadamu.
- II. Adamu maana yake "Mwanadamu"
- III. Biblia inaeleza kuhusu mwanadamu juu mambo kadhaa.
  - A. Kuumbwa kwake.
  - B. Kuanguka
  - C. Gharika ambapo vyote hivi vimeelezwa juu ya mwamadamu kama ni jumla.
  - D. Kuitwa kwa Abraham (Ibrahimi na Uzao wake)
  - E. Rehema inaonyeshwa kwa watu kadhaa.
    1. Rahabu, Yos. 2.
    2. Ruth, Ruth. 1
    3. Watu wa Ninawi, Yona.
- IV. Lakini Mungu alitoa ufunuo kwa watu wake Israeli.

#### Mwili:

- I. Kulikuwa na safari Tatu Kwa Mababa Watatu.
  - A. Ibrahimi
  - B. Isaka.
  - C. Yakobo.

## II. Ibrahimu:

A. Historia ya Israeli inaanza na Ibrahimu.

B. Akaitwa " Baba wa Imani" Aliondoka Uru wa Ukaldayo kwenda asikokujua.

1. Uru wa Ukaldayo - (Mwa. 11:27-32)
2. Kutoka Uru mpaka Harani. (Mw. 11:27-12:4) Mesopotamia Kusini-ndipo palipokuwa nyumbani Ibrahimu.
3. Kanani - Mwa. 12:5-9 - Ibrahimu na mkewe Sara waliondolewa kutoka Harani. Kutoka harani waliambatana na Lutu Binamu yake- kwenda Kanani iliyokuwa chini ya Misri.
4. Misri, Mwa. 12:10-20.
  - a. Ibrahimu alienda kutafuta chakula.
  - b. Ibrahimu aliongopa - Sara ni dada yake.
  - c. Ibrahimu alifukuzwa na Farao baada ya kugundua.
  - d. Ibrahimu alirudi Betheli.
5. Hebroni - Mwa. 13:5-18.
  - a. Ibrahimu na binamu yake Lutu walitengana.
  - b. Lutu alichagua - Sodoma bonde ambalo lilileta baadaye maangamizi ya Sodoma na Gomora.
    1. Lilikuwa ni bonde zuri kwa mifugo.
  - c. Ibrahimu alichukua sehemu za miinuko kuzunguka Hebroni.
    1. Hapo ndipo alipokufa mkewe Sara.
    2. Alinunua mahali pa kumzika mkewe kwa Efroni Mhiti.
    3. Daudi alianza kutawala akiwa Mfalme katika Hebron.
    4. Uasi mbaya wa Absolomu ulianza hapa.
    5. Kwa mara ya pili Ibrahimu aliambiwa hapa kuwa ni "Rafiki" Mungu.
6. Vita vya wafalme, Mwa. 14.
7. Beersheba, Mwa. 20 - 25.
  - a. Baada ya maangamizi ya Sodoma na Gomora.
  - b. Hapa Ibrahimu aliungana na Abmeleki wa Gerali (Mwa. 26: 26 -33).
  - c. Katika siku za za Ahabu na Jezebeli, Eliya alipata kutoa sadaka hapa baada ya ushindi wake dhidi ya manabii wa Baali, (1 Fal. 19:3-4).
8. Moria - Mwa. 22.
  - a. Mahali alipotolewa Isaka kama sadaka.
  - b. Mahali palipokuwa pametulia mbali na mikiki ya shughuli za watu.
  - c. Mapokeo hudai Ibrahimu alikuwa katika "Nchi ya Moria".

## III. Safari za Isaka.

A. Maisha ya Isaka katika Biblia yameelezwa kwa ufupi zaidi kuliko mababa wengine.

1. Beer-Lahai-Rol (Mwa. 16:7, 13; 14; 24:62)

- a. Hapa ni mahali Malaika wa Bwana alipomtokea Hajiri kijakazi wa Sara (Mama yake Isaka,) wakati Hajiri anamkimbia mkuu wake.
- b. Yawezekana Isaka aliishi hapo.
- 2. Gerari (Mwa. 26:1-16)
  - a. Ni mahali ambapo Isaka alipata makaribisho mazuri kutoka kwa Mfalme wa Gerali Abimeleki.
  - b. Isaka aliongopa kuwa Rebeka ni Dada yake, mst. 7-11.
- 3. Rehobothi (Mwa. 26:23-33)
  - a. Isaka alifanya mapatano ya Amani na Wafilisti chini ya mfalme wao Abimeleki.
  - b. Mungu anarudia Ahadi yake juu ya Ibrahimu.
- 4. Hebroni (Mwa. 35:27).
  - a. Maisha yake ya mwisho aliyatumia akiwa HEBRONI.
  - b. Ni mahali alipofia na kuzikwa na wanawe Yakobo na Esau katika pango lilelile alilonunua Ibrahimu (makapela).

#### IV. Safari za Yakobo.

- A. Jina lingene la Yakobo ni Israeli.
- B. Baba wa makabila 12 ya Israeli.

### MAISHA YAKE YAKO KAMA IFUATAVYO KWA UFUPI.

#### I. BEER -SHEBA: (Mwa. 26:33 - 27-46).

- A. Yeye na pacha mwenzie walizaliwa (Esau)
- B. Alidanganya na kupata baraka za uzaliwa wa kwanza watu aliowadanganya watu wawili nao ni:
  - 1. Isaka.
  - 2. Esau.
- C. Alikimbilia Harani - Baada ya kugundulika kwa mjomba wake Labani.

#### II. BETHELI: (Mwa. 28).

- A. Alikimbia kulipizwa kisasi na Esau.
- B. Alipewa na Mungu maono ya kurudia kwa amani katika nchi aliyozaliwa.
- C. Aliona ngazi kutoka Mbinguni.
- D. Ndama kama mungu iliwekwa na Yeroboam I kuepusha watu kwenda Yerusalem hekaluni, Ufalme wa Israeli ulipogawanyika (Yuda na Israeli).

#### III. HARANI: (Mwa. 29:30).

- A. Alitumia muda mwingi hapo.
  - 1. Alitumia miaka 7 kwa msichana mzuri Raheli badala yake alipewa Lea ambaye hakuwa anavutiwa naye.
  - 2. Alifanya miaka mingine 7 kwa ajili ya Raheli tena.
  - 3. Alitumia maisha yake Harani kwa kuishi na mjomba wake Labani.

#### IV. MAHANAIMU: (Mwa. 32:1).

- A. Alitiwa moyo na malaika baada ya kuogopa kulipizwa kisasi na nduguye aliye mkosea miaka ishirini mapema.
- B. Ni mahali ambapo baadaye mwana wa Sauli Ishi - Bosheth alitawala, wakati Daudi akitawala Yuda kutoka Hebroni.
- C. Ni mahali ambapo kilitokea kifo cha mateso cha mtoto mzuri sana wa Daudi Absalomu.

V. PENUELI (Mwa. 32:22 - 32).

- A. Penueli maana yake ni "Sura ya Mungu."
- B. Alipambana na Malaika, Yakobo alifanywa kilema na kupewa baraka.

VI. SUKOTHI (Mwa. 33:17).

- A. Yakobo alipatana na nduguye Esau.
- B. Alijenga madhabahu kwa ajili ya furaha ya kupatana na nduguye.

VII. SHEKEMU - (Mwa. 33:18-34:31).

- A. Shekemu kwa sasa inajulikana kama - TELL-BALATA.
- B. Dina binti Yakobo alibakwa na Shekemu.
- C. Simeon na Lawi waliwaua wanaume wote wa Shekemu.

VIII. BETHELI: (Mwa. 35:1-15)

- A. Jina lingine - "Nyumba ya Mungu."
- B. Yakobo alirudia agano lake na Mungu.

IX. EFRATH.

- A. Jina lingeni ni Bethlemu (Mwa. 35:16-21).
- B. Maili 5 kusini ya Yerusalemu.
- C. Ndipo alipokufa Raheli wakati anajifungua mtoto Benjamini mtoto wa mwisho wa Yakobo.

X. HEBRON - (Mwa.35:27).

- A. Ni mahali ambapo Ibrahimu na Isaka waliwahi kukaa.
- B. Mahali ambapo Yusufu mwana mpendwa wa Yakobo aliuzwa na ndugu zake Utumwani kwa wa Ishimaili.
- C. Kulikuwa na njia kutoka Damascus kwenda Misri.

XI. KULE MISRI (Mwa. 45-49)

- A. Alikwenda kwa mwaliko wa Yusufu.
- B. Yusufu alikuwa waziri mkuu wa Misri.
- C. Aliishi katika Gosheni kule Misri - Sehemu ndogo lakini yenye rutuba sana.
- D. Mwili wa Yakobo uliwekwa dawa ulihifadhiwa na kuchukuliwa kwenda kuzikwa Hebroni - Makapela.

**SOMO LA TATU.**

## MISRI NCHI YA UTUMWA.

### I. Majina matano ya nchi.

- A. Kemu - Jina la zamanil ililoonekana kumbukumbu za zamani.
- B. Nchi ya Hamu - (Zab. 78; 51; 105:23; 106:22)
- C. Mizraimu -Mwa. 12:10-14 ff; 13:1.
- D. Rahabu - (Kiburi au Jeuri) Zab. 87:4; 87:10.
- E. Misri - Jina la sasa Jina iliyoitwa na Wayunani halikutumiwa kamwe hapo daima.

### II. Historia yake ya nyuma.

- A. Misri ni sehemu ya bonde refu la mto Nile.
- B. Bonde hilo limegawanyika katika sehemu mbili au wilaya mbili zilizoitwa " Nomes".
- C. Kila sehemu ilikuwa na mji mkuu wake ambao ulikuwa na hekalu la mungu kienyeji.
- D. Lugha yao ni ile ya Kiarabu.
- E. Farao wa kwanza kutawala pande zote mbili aliitwa Menesi na ndiye aliyeiunganisha nchi.
- F. Wamisri walipenda sana desturi zilizofanya ustaarabu wao udumu. Kama maandishi yaliyo jumuisha maeneo matatu.
  1. Logographic - kilaalama iliwakilisha neno.
  2. Syllabic - Herufi alama iliwakilisha hefu.
  3. Alphabetic - alama iliwakilisha sauti moja.
  4. Mambo ya dini - miungu.
  5. Katika ufalme wa 3 kulikuwa na kawaida ya kufanya "RE" kuwa ni mungu jua - Ilichukua miaka mingi kwa Wamisri. miungu mingi - kusherehekea Mungu mmoja.
  6. Wafalme wa Misri walijulikana kwa jina la Farao.

### III. JOGRAFIA YA MISRI.

- A. Mgawanyo wa nchi katika nyakati mbili za Wamisri zamani ulijulikana na Kufikiriwa vitu kamili. Historia yake ilianza wakati sehemu mbili zilipounganishwa na mfalme Menesi mwanzilishi wa ufalme kukawa na kuvaa taji mbili kuonyesha kuwa anatawala pande zote mbili za Misri.
  1. Misri ya Kaskazini (Juu) ilikuwa mahali mto unapoingia baharini na ilikuwa pambetatu.
  2. Misri ya Kusini (Chini) Bonde jembamba la mto Nile.
- B. Misri inaanzia kwanza kwenye maanguko ya mto Nile kusini mwa Jimbo la Nubia.
- C. Kwa upande mwingine wa mto Nile ni jangwa.
  1. Jangwa Shuri linaloendelea mpaka Palestina ya kusini.
- D. Ukubwa wa Misri ni 9,600 sq. mile kwa 13,000 sq mile.
- E. Mipaka ya Misri.
  1. Jangwa la Sahara - Magharibi.
  2. Bahari ya Mediteranea - Kaskazini.

3. Nubia - Kusini.
4. Bahari Nyekundu - Mashariki na jangwa.

#### IV. MTO MKUBWA NILE.

##### A. Ukweli kuhusu mto Nile.

1. Ni mto mrefu kabisa katika Africa.
2. Unaweza kuwa na urefu wa maili 4,000.

##### B. Chanzo chake.

1. Ziwa Victoria lina mchango mkubwa katika chanzo cha mto Nile.
2. Vilevile kuna vianzo vyake toka kwenye maziwa ya Kas. Mashariki na Afrika ya kati.
  - a. Nile Nyeupe -mto wenyewe wa asili.
  - b. Sobati - Karibu na asili ya mto yenyewe.
  - c. Nile Nyeusi - inatokea maili 200 Khartoum.
  - d. Nile Blue - katika Ziwa Tana kule Ethiopia inayoungana na Nile Nyeupe kule Khartoum.
  - e. Unapoingilia Nile blue hakuna mwingine unaoingia katika mdomo huo.

##### C. Midomo ya Nile.

1. Nyakati za zamani kulikuwa na midomo 7 nyakati za saa iko midomo 5 ya usafiri wa wazi Baharini.
2. Kuna milango mikuu miwili.
  - a. MASHARIKI - au Pelusiac.
  - b. MAGHARIBI - au Canaopic.
3. Gosheni - ilikuwa ni makao ya Waisraeli ilikuwa Kusini - Mashariki ya tawi la Pelusiac la Nile.

##### D. Zawadi ya Mto Nile.

1. Mara moja kwa mwaka hufurika.
  - a. Ndiyo chanzo cha maisha kule Misri.
  - b. Mahali popote maji yanapofika palikuwa na Neema.
  - c. Huwa mavuno tele na maji huwapo.
2. Mafuliko haya ya kila mwaka huanza 25/6 na yanadumu kwa muda wa miezi 3 maji kuwa juu ya nchi.
3. Mafuliko husababishwa na mvua za kila mwaka kutokea Afrika ya kati.

#### V. Sehemu muhimu katika Nchi ya Misri.

##### A. Misri ya Juu.

1. Memphis - Maili 10 kutoka Kairo ya sasa.
  - a. Mji mkuu wa zamani wa Misri.
  - b. Kuna maeneo muhimu ya Ki-Historia.
2. Heliopolis - au "ON"
  - a. Kama maili 20 kutoka Memphis.
  - b. Kiti cha kuabudia "mungu jua".
3. Rameses:
  - a. Mji katika jimbo la Gosheni.
  - b. Yawezekana mji huu ulijengwa na watumwa wa Ki-Israeli

(Kut. 1:11).

- c. Ulikuwa ni mji mkuu kati ya falme.
- d. Pia uliitwa Zoan.

4. Pelusium:

- a. Mashariki mwa mdomo wa mto Nile.
- b. Maili za Mashariki mwa Bandari ya Saidi.
- c. Iliaminiwa kuwa mji wa dhambi katika Biblia.

5. Alexandria:

- a. Ulianzishwa na Alexander Mkuu mwaka 332 K.K.
- b. Wayunani wengi waliozungumza Kiyahudi waliishi hapa.
- c. Ndipo walilpotokea LXX (Septuagint).
  - 1. Katika mji yote iliyoorodheshwa hapa ni Alexandria uliobakia hadi leo.
  - 2. Ni moja ya maajabu saba ya dunia.

B. Misri ya Chini:

1. Thebes:

- a. Pia unaitwa "NO" AU Hakuna au NO -AMON.
- b. Mji mkuu wa Misri ya juu kwa muda mrefu.
- c. Kulikuwa na hekalu la Amoni.

**SOMO LA NNE  
WANA WA ISRAEL.  
NCHI WALIZOSAFIRI NA SEHEMU WALIZOZUNGUKA.**

**Utangalizi:**

- I. Historia ya Misri inaanza pale ufalme wa juu na chini ulipoungana chini ya NAR - MER au MENES, farao wa kwanza wa Misri iliyoungana.
  - A. Mfalme alikuwa na Taji mbili kumaanisha kuwa ni mtawala wa Misri mbili.
- II. Kwa kiebrania Misri ilijulikana kwa jina la MIZRAIM.
- III. Yawezekana Waisraeli walianza kuondoka Misri mnamo mwaka wa 1225 -1447 BC.
- IV. MEMPHIS, ni mji mkuu wa zamani wa Misri ambao sasa unajulikana ni KAIRO.
- V. Mji maalumu wa kidini ulikuwani Heliopoli au "ON" kule Misri Jina hilo lilijulikana kama mji wa jua ulikuwa maalumu kwa mungu jua "RE".
- VI. RAAMSES au RAMESES.
  - A. Mji wa kuanzia safari ya Waisraeli.
  - B. Ulikuwa katika jimbo la Gosheni.
  - C. Ulijengwa na watumwa wa Ki-Israeli.
  - D. Palikukuwa ni mahali Waisraeli walipoanzia safari kwenda Kanaani, (Kut. 12:37).

**Mwili:**

- I. Nyikani Walimozunguka Zunguka Waisrael.
  - A. Nyikani hapa yaweza kuwa inaelezea kila namba ya majangwa au nyika katika kuzunguka nchi za Biblia.

B. Kuna maana tofauti ya neno "nyika" kama lilivyo neno "jangwa" kuwa na maana tofauti za majangwa au nyika.

1. MIDBA - Nchi ya Nyika, (Mith. 21:19).
2. YESHIMONI - Nchi ya Ukame (Kum. 32:10).
3. ARABA - Nchi ya Chumvi, (Ayu. 39:6).
4. ISIYYAH - Nchi kavu isiyo zaa chochote, (Ayu. 30:3).
5. TOHU - Nyika msimo na njia, (Ayu. 12:24).
6. EREMIA -Ukame.
7. EREMO -Jangwa na Ukame.

## II. Majangwa Waliyozunguka.

A. Mkono ya Sinai na Majangwa Yake.

1. Walitumia karibu miaka 39 au 38 kwa kuzungukazunguka eneo hili.
2. Kumbuka lipo kati ya Ghuba ya SUEZ na Ghuba ya Agaba katika mikono miwili ya Bahari ya Shamu au Nyekundu.
3. Ilikuwa na maeneo tofauti mawili.
  - a. TAMBARALE - (Table - Land) - Chokaa, kame jangwa.
  - b. MILIMANI au miinuko - liliitwa kwa jina lingine Horeb au Sinai - kulikuwa na milima ya aina mbili
    1. Kas- Magh - 679 fts.
    2. Kundi la kati 7519 fts Mlima Sinai.

## II. Maeneo ya Jangwa Au Nyikani.

A. Maeneo matano ya safari ya wana wa Israeli ni majangwa.

1. Shuri - Mashariki mwa Gosheni maana yake ni " Ukuta"
2. Zini - Kus/Magh mwa Bahari mfu lipo katika nchi ya Edom. Iliyotwa wana wa Israeli walinung'unika, Hes. 27:14, wapelelezi alitumiwa Kanaani, Hes. 13:21.
3. Sini - Ipo kati ya Elimu na mlima Sinai - Magharibi ya mkono mashariki kati ya mkono ya Sinai.
4. Parani - Ipo kati ya mpaka wa Araba na Ghuba ya Agaba, Hes. 10:12.
5. Etham - Kusini mwa jangwa la Shuri ni sehemu ya mkono ya ya Sinai.

B. Hizi nisehemu chache muhimu katika safari ya wana wa Israeli.

1. Zilikuwa sehemu ya Kaskazini na kati ya Peninsula.
2. Eneo hilo ni tambarale.
3. Kulikuwa na vyanzo vichache sana vya maji hata mto Wad-El- Arish (Mto wa Misri) unakauka karibu kwa mwaka

mzima.

C. Mlima Sinai:

1. Unahusiana na jina la sehemu ya Sinai.
2. Horebu ipo sehemu ya kusini ya Peninsula ya Sinai.
3. Panajulikana kuwa ndipo mahali Musa alipopokea Sheria.
4. Kilele chake kimeitwa na wasomi wa Biblia kwa Kiarabu "JEBEL MUSA" yaani "Mlima wa Musa."



#### D. ARABA:

1. Kutoka kusini mwishoni mwa Bahari mfu mpaka Ghuba ya ya Agaba.
2. Waamaleki waliishi hapa na kuishambulia Israeli, (Kum. 25:17 19; Kut.17:8-16. wana Esau, Mwa. 36:16, 12).

#### III. Nchi Ya Edom:

##### A. Mipaka yake.

1. Kusini mash, ya Palestina katika jimbo la Kusini mwa Bahari Mfu, kati ya mto Zeledi na ghuba ya Agaba.
2. Asili ya milima hiyo ya mashariki mwa Araba ilipewa jina Ki-Biblia "MILIMA YA SEIRI."

##### B. Majina ya Nchi yalikuwa Matatu (Mwa. 36:8, 20).

1. Esau au Edomu - Mwekundu.
2. Seiri - (Hairy) - Nywele nyingi.
3. Idumea- ilitumika katika A.J. kati ya Uyunani - Herode alikuwa Mfalme wa Idumea.

##### C. Miji mikubwa mitatu ya Edomu.

1. Bozra - ulikuwa mji mkuu hasa katika A.K.
2. Sela - uliitwa Petro (Jiwe) na Wayunani - ulikuja kuwa mji mkuu baadaye.
3. Ezioni - Geberi:
  - a. Kusini mwa Edomu katika Ghuba la Agaba.
  - b. Njia kuu za kibiashara zilikuwa huku.
  - c. Njia hizi zisababishwa na Biashara ya Misri na Bonde la Frati.
  - d. Sulemani alitumia mji huu kama Bandari.

##### D. Sura ya Nchi.

1. Magh - kulikuwa na miinuko ya mawe chokaa.
2. Mash - kulikuwa na Slop ya mawe ya chokaa mpaka jangwa.
3. Kati - Nchi ya milima na aina mbalimbali za mawe zaidi ni mawe ya chokaa.

##### E. Mwisho wa Taifa hili la Edomu.

1. Historia hii ya Waedomu ni ya kuvutia sana
  - a. Esau nduguye Yakobo alishinda na kuteka nchi.
2. Waisrael (Yakobo) walipotoka Misri Waedomu waliwakatalia wasipite katika nchi yao, Hes.20:17-21.
3. Daudi na Sulemani baadaye waliunganisha nchi hii na miliki yao.
4. Kufuatia kipindi cha Ufalme uliogawanyika kati ya Israel na Yuda (Kas. na Kus.) Edomu ilifanywa sehemu ya Yuda.
5. Edomu iliasi na kujitawala wenyewe.
6. Babeli (Nebukadneza) alipoishambula Palestina Edomu ilimsaidia (Kitabu cha Obadia).
7. Wakati wa Makabayo Idumea au Wa-Edomu walilazimishwa kuungana tena na kuwa chini ya sheria za Wayahudi.
8. Haipo katika historia ya sasa kufuatia maangamizi ya Yerusalemu ya

70. B.K. Mat.24:1-35.

a. Hakuna nchi inayoitwa Edomu leo.

IV. Njia na Vituo Vya Wana Wa Israeli - Kuzunguka Kwao Jangwani.

A. Kwa nini walikwenda kwa njia waliyoiendea? Kwa nini wasipite moja kwa moja kwenye pwani ya Mediteranea? Na kuvuka mto Wadi-el-Arishi (Mto wa Misri) na kutembea mpaka Kanaani? Kuna sababu 4 tunazoweza kuzielewa.

1. Ulikuwa ni mpango wa Mungu. (Kut.13:17, 18).

a. Wafilisti wangepigana na Israel ... Kwa hiyo wangekata tamaa.

2. Njia ya Pwani ilikuwa na ngome nzito ya Askari wa maadui.

3. Jangwani ilikuwa imethibitishwa kwa safari.

4. Hawakuwa tayari kukabiliana na Wafilisti.

B. Njia zinazofanya kuwa Historia.

1. Rameses, Mahali walipoanzia katika Goshen, (Mwa.37:27; Kut. 12:37)

2. Sakothi - Israel walijiunganisha, (Kut. 12:37 -3:19) Hapa walikuwa wanaingia katika Jangwa la Ethamu.

3. Kwenye Pembe ya Jangwa la Ethamu.

4. Pi - Hahirothi - (karibu na Baal-Sefoni), Kut. 14:4-15:22

a. Farao aliwafuata alitaka kuwarudisha Misri.

b. Muujiza wa Mungu uliigawanya Bahari ya Shamu.

c. Vituo hivi vinne vyote vilikuwa katika nchi ya Misri na juu ya Bahari ya Reeds (Shamu).

d. Sasa katika Jangwa la Shuri.

5. Maji machungu ya Mara yaligeuzwa kuwa matamu, (Kut. 15:22-26)

6. Elimu:

a. Palikuwa na miti ya mitende 70.

b. Chemichemi ya visima 12, (Kut. 15:27). Sasa katika Jangwa la la Sini.

7. Walipofika hapa Sini watu walimnung'unikia Mungu na Musa na Mungu aliwalisha watu.

a. Mikate-manna.

b. Kwale-(Kut. 16:2-36)

8. Refidimu kwa sababu ya mateto mahali hapo Musa lipaita MASA NA MERIBA, (Kut. 17:7).

a. Maji kutoka katika mwamba.

b. Vita dhidi ya Wa-Amaleki.

c. Mikono ya Munsu ilitengenezwa na watu wawili.

1. Haruni.

2. Huri.

d. Mungu aliahidi kufuta kabisa Amaleki juu ya nchi.

e. Musa aliambiwa aandike kwa ajili ya Yoshua.

f. Musa alijenga madhabahu akaiita Yehova - Nisi maana yake Bwana ameapa kutakuwa na vita na Amaleki kizazi hadi kizazi Kut. 17:15-16.

9. Sinai, (Kut. 19:1-40:37)

- a. Walawi wote na Hes, 1:1-10:11.
  - b. Sura ya 19- 24-Sheria zinatolewa.
  - c. Sura ya 25-31-Kielelezo cha Hema.
  - d. Sura ya 32- 34-Ibada ya sanamu.
  - e. Sura ya 35-40-Ujenzi wa Hema.
- \* Sasa tunaacha Sinai na kwenda kwenye kichwa cha Kadesh-Barnea.
10. Tabera (Unguza) Hes. 11:1-3.
- a. Watu walinung'unika.
  - b. Moto wa Bwana uliwala baadhi yao.
11. Kibroth - Hataava - (Kaburi la Tamaa)
- a. Wote waliotamani Misri Mungu aliwapiga hapa.
12. Haserothi-Hes. 11:4-34.
- a. Miriamu na Haruni walimnenea vibaya Musa kwa sababu ya mkewe Mkushi.
  - b. Miriamu alipingwa na ukoma, Mst.10.
  - c. Haruni aliomba msamaha, Mst. 11.
- \* Sasa wanaingia katika Jangwa la Parani, Hes.12:16.
13. Kutoka Kadeshi- Barnea.
- a. Wapelelezi 12 waliingia Kanaani.
    - 1. Wapelelezi 10 walaminiwa, (Hes.13:1-14:45; 13:26.
- \* Katika kipindi hiki walipita Jangwa la Sini mpaka Hamathi.
14. Kuna vituo 12 visivyofahamika.
- a. Kwa miaka 38 walikuwa wakizunguka Jangwani.
  - b. Hes. 15-19 Biblia imenyamaza.
  - c. Vituo 12 vimeorodheshwa katika, Hes. 33:18-38.
    - 1. Wanapewa maagizo na mwelekeo, Hes. 15.
    - 2. Maasi yanatokea , Hes. 16-Kora Dathanina Abiramu.
    - 3. Fimbo ya Haruni inachipuka, Hes. 17:11, kuwa ushahidi
    - 4. Kufuatana na makuhani na walawi, Hes. 18.
    - 5. Maagizo ya mtamba mwekundu, Hes. 19.
15. Kadesh - Barnea: Hes. 20:1-20. (katika Jangwa la Zini.)
- a. Mahali alipofia Mariamu, (dada yake Musa.)
  - b. Mahali Musa alipopiga Mwamba.
  - c. Baadhi ya walionungu'unika waliteketezwa kwa moto, Hes. 11:1-3.
  - d. Waedomu wanawazuia Israel wasipite katika nchi yao, Hes. 20:21.
16. Walifika mlima Hori.
- a. Mahali alipofia Haruni.
  - b. Vita dhidi ya Wakaanani.
  - c. Watu walikufa moyo kwa sababu ya ile njia, Hes. 21:4.
    - 1. Walitamani kurudi Misri.
    - 2. Hawakutaka kufa jangwani.
    - 3. Walikinahiwa na chakula kutoka kwa Bwana (Kwali na mikate).
    - 4. Nyoka wa moto waliwauma Mungu akamwambia

Musa atengeneze nyoka wa shaba.

5. Walirudi tena Bahari ya Shamu (Agaba).

17. Elathi:
- a. Watu waliumwa na kufa kwa nyoka za moto, Hes. 21:4, 9; Kum.2:8.
18. Esion- Gebari : Kutoka hapa walianza kuizunguka Nchi ya Edomu mashariki mwa mto Jordani, Kum. 28.
19. Bonde la Moabu: Hes. 21:10-22, Mfululizo wa matukio tutayaona.
- a. Musa na Haruni-wanadai kuwapa watu maji, Hes. 20:8-13.
  - b. Waliwaita watu enyi waasi, Hes. 20:10.
  - c. Baadala ya kuuambia mwamba Musa anaupiga, 20:11.
  - d. Bonde la Zeredi - Musa na Haruni hawakumtukuza Mungu.
  - e. Ng'ambo ya Arnoni.
    1. Maji yaliitwa Meriba - Wana wa Israeli waliteta na Bwana.
  - f. Beer. Wanaomba ruhusa kwa Edomu kupita katika nchi yao.
  - g. Mattaha- Edomu anataka kupigana na Israeli.
  - h. Israel walibembeleza sana, hatuta kunywa maji yako wala mifugo yetu, mst. 18, bado Edomu hakuwa ruhusu.
  - i. Bonde la Moabu, Hes. 20:20; Yos. 4:19.
    1. Sihoni - Mfalme wa Wa-Amori, Hes. 20:21-23 walishindwa na Israel Og - mfalme wa Bashani.
    2. Uasi na manung'uniko, Hes. 22:1-26:1.
    3. Watu walihesabiwa, Hes. 26:2 -26:65.
    4. Sheria mbalimbali, Hes. 27:1-31:2.
    5. Vita na Wamidiani, 31:3-54.
    6. Marudio na mgawanyo wa Nchi, Hes. 32:1-36:13.
    7. Kifo cha Musa, Kum. 34:1; Yos. 1:2.
    8. Kazi ya Yoshua, Yos. 1:3-18.
    9. Kuipeleleza Nchi, Yos. 2:1-24.
    10. Maji ya mto Yordani yalitindika. Miili 2 ya maji iliyowa kutindika.
      - a. Bahari ya Shamu.
      - b. Mto Yordani, Yos. 3:18.
  - j. Gilgali: Vita katika Kanaani mwisho wa safari ushindi uanaanza.
    1. Vita katika Kanaani vinaanza.
    2. Mwisho wa Safari (Kituo cha Mwisho).
    3. Ushindi unianza kupatikana.

### **SOMO LA TANO.**

### **USHINDI WA KANAANI.**

#### UTANGULIZI:

I. Makabila yaliyokuwa Kanaani wakati wa Mababa na waliopaswa kushindwa na kutoka

mbele ya Israel, Kumb. 7:8 - sura ya 8.

- A. Mhiti - Uria - 2 Sam.11:1-27; Heth, Mwa.10:15.
- B. Mgirgashi.
- C. Mwamori.
- D. Mkanaani.
- E. Mperizi - Vijijini.
- F. Mhivi.
- G. Myebusi - Wakaani walioshi Yerusalemu.

II. Makabila au mataifa yaliyokuwa yakiishi wakati Waisrael walipokuwa wanateka Kaanani.

- A. Moabu - Mwa. 19:30-37 - Wajukuu wa Luthu.
  - 1. Waliabudu. Kemoshi - Kuchoma watoto hai katika moto.
- B. Ammoni - Hawa nao ni wale walitokana na Luthu, Mwa. 19:30- 38.
  - 1. Mungu wao alikuwa. Moleki au Mikom.

III. Ushindi wa Kanaani ulikuwa kabla ya wana wa Israeli kufika katika kituo chao cha Mwisho.

- A. Kituo chao cha mwisho kilikuwa - Gilgali.
- B. Ilikuwa washinde mashariki ya Yordani kabla ya kuingia katika Nchi yenyewe.
- C. Walipoiona Nchi waliigawanya miongoni mwa makabila.

### Mwili:

I. Ushindi wa Mashariki, Hes. 31:54.

- A. Vita dhidi ya Sihoni wa Gileadi - Hes. 21:21-31.
  - 1. Mfalme wa Amorite (Mwamori) alikuwa mpinzani sana wa Israel.
  - 2. Amorite (Waamori) waliwafukuza mbali Wamoabu.
  - 3. Kulikuwa na makundi mawili ya Waamorite.
    - a. Geliadi -Sihoni.
    - b. Bashani - OG.
  - 4. Kundi la Gileadi - lilikuwa kati ya Arnoni na Jabbok.
  - 5. Mji wao mkuu ulikuwa - Hesh. - Boni au Eseboni.
- B. Vita dhidi ya OG wa Bashani, Hes. 21:32- 35.
  - 1. Kaskazini ya mto - Yamuku.
  - 2. Mgawanyo wa Waamori.
  - 3. Mtawala jina lake OG.
  - 4. Vita vilipiganiwa Edrei.
  - 5. Nchi ilisherehekea vitu vifuatavyo.
    - a. Ng'ombe.
    - b. Kondoo.
    - c. Mti wa ulaya unaoshi mufa mrefu.
- C. Vita dhidi ya Moabu na Midiani, Hes. 22:31-37.
  - 1. Moabu na midiani waliungana kijeshi, 22:4.
  - 2. Moabu ilikuwepo kati ya Zeredi na Arnoni.
  - 3. Midiani ilikuwa mbele ya kona ya Jangwa la Arabia.
  - 4. Mji mkubwa - Kir-Moabu.
    - a. Wamoabu - Luthu - Binti mkubwa, Mwa.19:30-37.

b. Waamoni - Luthu - Binti mdogo, Mwa.19:30-37.

## II. Magharibi (Kuyasukumia mbali), Yos. 1:1 - 11:23.

### A. Vita vya katikati, Yos. 3 - 9.

1. Gilgali - kituo muhimu.
2. Yeriko - (mji wa mwezi au mji wa mitende).
3. Ai. - walishindwa kwa sababu ya dhambi ya Akani.
4. Bethel - (Ai waliamini kuwa ni kutuo chao cha kijeshi).
5. Milima Gerizimu na mlima Nebo, (Kum. 27:11 ff, Yos. 8:32).

### B. Vita vya Kusini. (Yos.10:1- 43)

1. Kuanguka kwa Yeriko, Ai, Amani na Gibeoni kuwa Kanaani.
2. Ushirikiano ulioundwa ilikupigana na Israeli, Yosh. 10:5, 15-26.
3. Ushirikiano wa kumshambulia Gibeon.
4. Yoshua alikwenda kwa nguvu na kushambulia usiku, Yos. 12:9-24.

### C. Vita vya Kaskazini, Yos.11:1-23.

1. Muungano mwengine wafalme uliongozwa na Yabini mfalme wa Hazori uliundwa kupigana na Israeli.
2. Yoshua alikwenda kwa njia ya Bonde la Yordani akashambulia.
3. Yoshua aliuchoma mji wa Hazori na akaiacha miji mingine.
  - a. Kwa nini Hazor, Yoshua aliuchoma moto? Malme wake alikuwa mwanzilishi wa muungano wa kuipiga vita Israeli.
4. Ushindi kimsingi ulikuwa umefikiwa lakini ghasia ziliendelea, Yos. 11:15- 23.

## III. Mgawanyo wa Nchi kati ya Makabila 12.

### A. Mashariki ya Yordani- Makabila 2 na nusu, Yos. 13.

### B. Magharibi ya Yordani - Makabila 9 na nusu, Yos. 14-19.

### C. Miji ya Makimbilio sita.

1. Mtu aliye ua mtu.
2. Aliyeua bila kukusudia, Yos. 20.
3. Miji hiyo ilikuwa kama ifuatavyo.
  - a. Katika pande zote.
    1. Upande wa Yordani Mashariki.
    2. Upande wa Kusini.
    3. Upande wa Kati.
    4. Upande wa Kaskazini.
  - b. Yordani Mashariki, mst.8.
    1. Bezeri - Rubeni.
    2. Ramothi - Gadi.
    3. Golani - Manase.
  - c. Magharibi ya Yordani, mst. 7.
    1. Hebroni - Yuda.
    2. Shekemu - nusu Manase.
    3. Kadeshi - Naftali.

### D. Miji ya Walawi, Yos. 21.

1. Ilikuwa 48, pamoja na miji 6 ya makimbilio.

2. Wastani ilikuwa miji 4 katika kila kabila.
- E. Maelezo zaidi walivyokaa katika nchi, (mgawanyo wa nchi kufuatana na makabila).
  1. Mashariki mwa mto Yordani yalipewa makabila 2 na nasu kukaa lakini ilikuwa wawasaidie waliobakia kushinda vita baadaye kurudia katika nchi yao, Yos. 22.
  2. Makabila hayo yalikuwa:
    - a. Reubeni.
    - b. Gadi.
    - c. Nusu Manase.
  3. Magharibi ya mto Yordani (Palestina halisi).
    - a. Kabila za kusini.
      1. Yuda.
      2. Simeon.
      3. Benjamini.
      4. Dani.
    - b. Kabila za kati kati.
      1. Efraimu.
      2. Nusu Manase.
      3. Isakari.
    - c. Kabila za Kaskazini.
      1. Asheri.
      2. Zebuluni.
      3. Naftali.

**SOMO LA SITA.**  
**PALESTINA CHINI YA WAAMUZI.**

**Utangulizi:**

- I. Baada ya kifo cha Yoshua sehemu fulani ya Israeli walikuwa kawaida ya kujiingiza katika sanamu na kuabudu miungu kama walivyokuwa wanafanya majirani zao.
- II. Tunajifunza katika historia kuwa Mungu aliwaokoa watu kutoka kwa maadui zao.
- III. Mungu aliwainua viongozi ili kuwaokoa watu na wale waliokuwa wakiwatesa.
  - A. Viongozi hawa walijulikana kama waamuzi.
  - B. Walikuwa tofauti na wafalme waliokuwa wakiwaacha watoto wao kiti cha Ufalme.

**Mwili:**

- I. Wakati wa maamuzi Israeli ilikuwa na vita vingi.
  - A. Vita kati yake na Mesopotamia - (Waa. 3:5-11).
    1. Mwamuzi alikuwa Othnieli-Yos. 15:16-19; Waa. 3:9-10.

- a. Ndugu yake Kalebu.
  - b. Amani ilikuwa miaka 40.
  - B. Vita na Wamoabu - (Waa. 3:12-30)
    - 1. Mwamuzi alikuwa -Ehudi - kutoka kabila ya Benjamini Amani ilidumu miaka 80.
  - C. Vita na Wafilisti- Maa. 4- 5.
    - 2. Mwamuzi au mwokozi - Shamgari (Maa. 3:31).
  - D. Vita na Wakanaani (Maa. 4-5)
    - 1. Mwamuzi au mwokozi - Yabini - Yos. 11:1
  - E. Vita na Wakaanani tena - Maa. 4:4 ff.
    - 1. Mwamuzi au mwokozi - Debora mwanamke pekee mwamuzi alisaidiwa na Baraka, Waam. 4:10, Debora na Baraka walifanya Israeli kukaa katika Bonde la Yezerel bila hofu ya Wakanani.
  - F. Vita na Wamidiani - Waa. 6-9, mwamuzi ni Gideoni.
    - 1. Gideoni na watu 300 alilishinda jeshi kubwa la Wamidiani.
  - G. Vita wa - Ammoni - Wajukuu wa Luthu, (Maa. 10-11).
    - 1. Mwamuzi alikuwa ni Yeftha.
  - H. Vita na Wafilisti tena: Maa. 13-16.
    - 1. Mwamuzi alikuwa ni Samsoni.
  - I. Mwamuzi wa mwisho kati ya wengi wa Israeli alikuwa Samweli.
    - 1. Israeli walitaka kuwa na mfalme kama majirani zao-mataifa, 1 Sam. 8:1 ff.
    - 2. Kitu hiki hakikumpendeza Samweli hata Mungu hakupendezwa na madai yao.
- II. Baada ya waamuzi wote kupita na Israeli kudai wawe na mfalme, bonde vita viliendelea moja baada ya vingine.
- A. Sauli ndiye aliyekuwa mfalme wa kwanza wa Israeli iliyo moja. (Monarch)
    - 1. Alipakwa mafuta kule Ramatahaimu au Ramali kwa siri nyumbani kwa Samweli.
    - 2. Alitokea katika kabila dogo sana la Benjamini.
    - 3. Gibeaa- kulikuwa ni myumbani kwa Sauli na makao makuu ya mfalme wa kwanza wa Israeli.
    - 4. Uko maili 4 kaskazini mwa Yerusalemu.
    - 5. Mizpeh - Sauli alipokelewa kama mfalme.
    - 6. Gilgali - kwa mara ya kwanza Sauli alipokilewa kama mfalme wa makabila yote ya Israeli.
- III. Vita vya Sauli, (1 Sam. 11-15).
- A. Vita vilikuwa kati ya mataifa yafuatayo:
    - 1. Waamoni - 1 Sam. 11.
    - 2. Vita vya kwanza na Wafilisti - (1 Sam. 13-14.)
    - 3. Vita na wamoabu - 1 Sam. 14:47.
    - 4. Vita na wa Edomu - 1 Sam. 14:47.
    - 5. Vita na Shemu, 1 Sam. 14:47.
    - 6. Vita na Waamaleki, 1 Sam.14:48 - 15:35, hasira za Samweli ziliinuka



kwa sababu Sauli alimwacha Agagi mfalme wa Waamaleki aliwaacha ng'ombe wazuri, 1 Sam. 14:22-23.

7. Vita vya pili na Wafilisti, (1 Sam. 17:18).

B. Sauli aliuawa katika vita na Wafilisti pamoja na wana wake watatu akiwemo Yonathani katika mlima Giboa.

#### IV. Ufalme wa Daudi na Sulemani.

A. Daudi alipokuwa mfalme wa Israeli walikuwa na wajibu na miliki 6000 maili za mraba.

B. Aliacha maili 60,000 za mraba kwa mwanawe Sulemani.

C. Utawala wa Daudi juu ya Yuda, 1 Sam. 1-4.

1. Baada ya kifo cha Sauli, Daudi aliondoka kwenye mji wake wa ukimbizini wa Ziklag na kwenda Hebroni kule aliko tangazwa kuwa mfalme wa Yuda.

2. Wakati huo mwana wa Sauli Ish - Boshesh alikuwa anatawala makabila ya Kasikazini.

3. Mapigano yalizuka kati ya majemedari wa Daudi na Ish-boshesh. Aliuawa na watu wake pamoja na Jemedali wake hivyo Daudi akawa Mfalme wa Israeli yote.

#### V. Ushindi wa Daudi kwa Mataifa - Kigeni. (2 Sam.8:11).

A. Aliteka mji wa Wa-yebusi wa Yerusalemu akaufanya makao yake makuu.

B. Kisha alishinda Kaskazini ya Palestina (Kanani) miji aliyoteka Kaskazini ni kama ifutatavyo.

1. Megido.

2. Taanaki.

3. Beth-Sheani.

C. Aliteka tena nchi zifuatazo upande wa Mashariki ya Yordani.

1. Edomu, 2 Sam. 8:13-14.

2. Moabu, 2 Sam. 8:2.

3. Amoni, 2 Sam. 10-11.

D. Yawezekana hata wafilisti na wenyeji wa Aramu - Dameski walimtumikia Daudi, 2 Sam. 8:5, 6.

E. Aliteka Soba, 2 Sam. 3-5.

